

## **Changamoto zinazowakumba vijana katika tamthilia ya Kitumbua kimeingia mchanga**

Katika ulimwengu wa sasa, kuna mabadiliko chungu nzima yanayoshuhudiwa duniani kote yanasababishwa na masuala anuwai kama vile maendeleo ya kiteknolojia pamoja na utandarithi yanayoathiri pakubwa maisha ya vijana. Hapo nchini, vijana wana umuhimu wa kipekee kwani wanatekeleza majukumu muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi. Isitoshe, idadi ya vijana kote ulimwenguni imeendelea kuongezeka kila uchao na imepiku ile ya wazee. Kwa hivyo, ni nyema kujadili changamoto zinazowakabili na kupendekeza hatua za kukabiliana nazo. Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchanganua changamoto zinazowakumba vijana pamoja athari zake katika ya tamthilia ya Kitumbua Kimeingia Mchangaya S.A Mohamed (2000). Mada hii ilichaguliwa kwamba vijana wanakumbwa changamoto nyingi katika maishayao zinazowaathiri kwa kiasi cha haja na kutinga juhudi za kuafikia jaala zao. Utafiti huu ulilenga kubainisha changamoto zinazowakumba vijana katika tamthilia hii na kutambua mbinu ambazo vijana hawa wanazua ili kukabiliana nazo. Nadharia ya Uhalisia ilitumika kwa sababu ilionekana kufaa zaidi kuchanganua changamoto zinazowakumba vijana kwani changamoto hizi zina uhalisia mkubwa katika maishayao. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchunguzana kueleza namna changamoto za vijana zinavyojitokeza katika tamthilia ya Kitumbua Kimeingia Mchanga na kisha kubainisha hatua zinazochukuliwa kuzitua changamoto hizo. Utafiti huu ni wa kimaielezo na kiudhamano kwani ulihusisha kuchanganua matini zinazohusiana na mada husika. Sampuli katika utafiti huu ilituuliwa kimakusudi kwani ndiyo ingempa mtafiti data aliyonua kuipata. Utafiti huu ulijikita katika maktaba ya kitaifa na yale ya vyuo vikuu humu nchini. Utafiti wetu umebainisha kidakidaki kwamba tamthilia ya Kitumbua Kimeingia Mchanga imesheheni Changamoto nyingi mno zinazowaathiri vijana kamavile dawa za kulevya, dhuluma, anasa, uavyaji mimba, utabaka, athari za tamaduni zakiigenipamoja nakufanyiwa uamuzi. Aidha, imethahirika wazikuwa vijana wanazua mbinu kabambe za kutatua changamoto zinazowakumba kama vile kutafuta ushauri kutoka kwa wenzao, kutumia wazee na kuwa na ujasiri wa kujitetea dhidi ya wanaowadhulumu pamoja na serikali kukabiliana na walanguzi wa dawa za kulevya. Ni bayana kuwa utafiti huu utafaa jamii ya wasomi wanaoshughulikia maswala ibuka katika jamii. Inapendekezwa kuwa tafiti za baadaye zitafiti kuhusu nafasi ya vijana katika jamii.